# Ulega aagiza wanaouza mazao ya uvuvi wasibughudhiwe

**Na Fadhili Abdallah, Kigoma**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka wasimamizi wa rasilimali za uvuvi kuacha kuwabughudhi wafanyabiashara wanaouza mazao ya uvuvi kwa kigezo cha kukamata dagaa na samaki wasiostahili kuvuliwa.

Ulega alisema hayo akizungumza na wavuvi katika mwalo wa Katonga Manispaa ya Kigoma Ujiji ambako alikumbana na malalamiko ya wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi kukamatwa na kutaifishwa mali zao na kikosi cha doria.

Alisema kuwa wafanyabiashara hao wachuuzi ambao wengi wao ni wanawake si wanaoingia ziwani kuvua na badala yake walinzi wa rasilimali za uvuvi na vikosi vya doria wapambane na wavuvi ambao wanajua sheria na taratibu za uvuvi ikiwa ni pamoja na kujua ukubwa wa dagaa na samaki wanaopaswa kuvuliwa.

Alisema kuwa serikali imejiandaa kuhakikisha inawawekea mazingira mazuri wavuvi na watu wanaoshughulika na mazao ya uvuvi kupata mikopo ya kuboresha shughuli zao.

Akitoa taarifa kwenye ziara hiyo, Msimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Ziwa Tanganyika, Juma Makongoro alisema kuwa doria zinazofanywa na ofisi yake zimesaidia kupunguza uvuvi haramu kwa kiasi kikubwa katika ziwa hilo.

Makongoro alisema pamoja na kupunguza uvuvi haramu, pia imesaidia kuongeza mapato ya serikali ambapo kwa mwaka wa fedha uliopita waliingiza Sh bilioni 1.8.

Mwenyekiti wa Wavuvi Mwalo wa Kibirizi, Paulo Samuel alisema wizi wa zana za uvuvi unaofanywa na maharamia unarudisha nyuma juhudi zao za kuendeleza shughuli zao.

Scanned with CamScanner

# Ulega awashukia wanaosumbua wafanyabiashara wa samaki

Na FADHILI ABDALLAH, *Kigoma*

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wasimamizi wa rasilimali za uvuvi, kuacha kuwasumbua wafanyabiashara wanaouza mazao ya uvuvi kwa madai ya kukamata dagaa na samaki wasiostahili kuvuliwa.

Badala yake amesisitiza uwekwe utaratibu wa kuwakamata wavuvi wanaokiuka sheria za uvuvi.

Ulega alisema hayo juzi wakati akizungumza na wavuvi katika mwalo wa Katonga, Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambapo alikumbana na malalamiko ya wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi kukamatwa na kutaifishwa mali zao.

Alisema wafanyabiashara hao ambao wengi ni wanawake, hawaingii ziwani kuvua, hivyo walinzi wa rasilimali za uvuvi na vikosi vya doria wapambane dhidi ya wavuvi ambao wanajua sheria na taratibu za uvuvi.

Naibu waziri huyo alisema kwamba, serikali imejiandaa kuhakikisha inawawekea mazingira mazuri wavuvi na watu wanaoshughulika na mazao ya uvuvi, kupata mikopo ya kuboresha shughuli zao ili ziwe na tija katika kukuza uchumi, kutoa ajira na kuingiza mapato ya kutosha kwa serikali.

Akitoa taarifa katika ziara hiyo,

> **Sinopharm ni moja ya chanjo za Uviko-19 zilizoidhinishwa na Shirika la Afya duniani (WHO) kwa ajili ya mapambano ya ugonjwa huu.**
>
> Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka.

Msimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Ziwa Tanganyika, Juma Makongoro, alisema doria zinazofanywa na ofisi yake, zimesaidia kupunguza uvuvi haramu kwa kiasi kikubwa katika ziwa hilo.

Makongoro alisema pamoja na kupunguza uvuvi haramu, imesaidia kuongeza mapato ya serikali ambapo kwa mwaka wa fedha uliopita, waliingiza sh. bilioni 1.8.

Awali, Mwenyekiti wa Wavuvi Mwalo wa Kibirizi, Paulo Samuel, alisema wizi wa zana za uvuvi unaofanywa na maharamia kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), unarudisha nyuma juhudi zao za kuendeleza shughuli.

Pia, alisema ugumu wa kupata mikopo kutoka taasisi za fedha kwa masharti magumu unakwamisha juhudi zao za kuwa na zana za kisasa hivyo kuomba serikali kuwawekea mazingira rahisi ya kupata mikopo, ujenzi wa mwalo wa kisasa Katonga na kuondolewa kero na uchumu wenye kero kutasaidia kufanya shughuli yao kuwa na tija.

Scanned with CamScanner

ya mradi wa "Kama", unaotekelezwa na ... wa mafunzo yaliyofanyika katika kata ya Bugarama, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Samaki, dagaa kuwa mazao ya kimkakati

**Na Pendo Thomas,**
KIGOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imekusudia kupandisha hadhi dagaa na samaki wa Ziwa Tanganyika kuwa zao la kimkakati litakaloongezwa thamani na kuuzwa ndani na nje ya nchi hatua itakayochochea kukua kwa uchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akiwa mkoani Kigoma katika ziara yake ya kikazi.

Ulega alisema utekelezaji wa mpango wa dagaa na samaki kuwa zao la kimkakati utaendana na utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya uvuni.

"Hapa tuna mazao yetu ya kimkakati na tumeyadhamiria yapande hadhi na nyie tuungeni mkono. Tunataka yainue Kigoma, wavuvi wainuke pawe shime kabisa," alisema Ulega.

Aliema mpango huo utasaidia kuondoa tatizo la dagaa kuharibika hasa kipindi cha mvua ambacho hushindwa kukauka. Alisema mpango huo utaendana na uanzishwaji wa viwanda vya uchakataji utakaosaidia kupandisha thamani.

Paulo Samweli, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Mwalo wa Kibirizi, alisema wavuvi wameendelea kukumbana na vitendo vya ujambazi ndani ya Ziwa Tanganyika ambavyo vinapaswa serikali itoe utatuzi wa haraka ili kuwawezesha kuendelea kufanya shughuli zao kwa usalama.

Alisema matukio hayo yamekuwa yakitishia usalama wao pamoja na kuwarudisha nyuma kwa kuwa zana zao za uvuvi zimekuwa zikiporwa na majambazi, hivyo baadhi yao kusitisha shughuli hizo.

Pia aliiomba serikali kuwapatia mikopo yenye riba nafuu au isiyo na riba itakayowasaidia kununua zana bora za uvuvi ambazo zitaongeza uzalishaji.

Naye diwani wa Bangwe manispaa ya Kigoma Ujiji, Hamis Betese, aliomba uharakishwaji wa ujenzi wa mwalo wa Katonga ili wafanyabiashara wawe na sehemu nzuri ya kununua na kuuzia mazao ya uvuvi hatua itakayoongeza mapato ya serikali kupitia uvuvi.

Scanned with CamScanner

# 'Dagaa wa Kigoma kuwa zao la kimkakati'

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Kigoma.** Serikali imejipanga kuhakikisha dagaa wa Kigoma wanakuwa zao la kimkakati la kibiashara litakalovutia wawekezaji na kusisimua uchumi wa mwananchi na Taifa.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema hayo wakati akizungumza na wadau wa uvuvi katika Mwalo wa Katonga mkoani hapa juzi.

Ulega alisema Serikali itaondoa vikwazo vyote vinavyowasumbua wavuvi ili kufikia lengo hilo.

Akifafanua sababu ya Serikali kufanya dagaa wa Kigoma wanakuwa zao la mkakati, alisema ni kutokana na biashara hiyo kuhusisha watu wengi katika jamii na pia, itasaidia kuimarisha uchumi wa wananchi.

**"Serikali tunataka kuinua biashara ya dagaa wa Kigoma, tunataka wavuvi wainuke kiuchumi, tumejipanga kuondoa vikwazo vinavyowasumbua na tutalitangaza vyema zao hili ili kuvutia uwekezaji."**
**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega**

Aliwataka viongozi wa mkoa kuanza mikakati na kampeni maalumu ya kutangaza ubora wa dagaa ili kuvutia uwekezaji wa viwanda vidogo na vikubwa kwa ajili ya kuwachakata.

Alisema zao hilo likitangazwa vizuri, wawekezaji na taasisi za kibenki zitawekeza na huo ndio utakuwa mwisho wa dagaa wa Kigoma kutupwa ovyo kwa sababu ya kukosa soko.

Diwani wa Bangwe, Hamisi Besete alisema Serikali inapoteza mapato mengi kwa sababu Mwalo wa Katonga haujajengwa, hali inayosababisha wafanyabiashara wa samaki na dagaa kukosa maeneo ya kuuzia biashara zao.

Scanned with CamScanner

# Authorities in Muleba District pledge to fight illegal fishing in Lake Victoria

**By Correspondent Mutayoba Arbogast, Kagera**

AUTHORITIES in Muleba District, Kagera Region have vowed to fight illegal fishing in Lake Victoria and promote sustainable fishing for regional development and the country at large.

This follows a recent crackdown operation along coasts of Lake Victoria, which caught six suspects of illegal fishing at Mahiga beach, Iroba village in Bumbire Island.

Speaking when the suspects were brought at district's headquarters, Muleba District Commissioner, Toba Nguvila said illegal fishing will be fought with all efforts to ensure that there is legal and sustainable fishing in the Lake.

He ordered the suspects to be taken to court immediately to face their charges.

The suspects were found with three boats, 15 pieces of illegal fishing driftnets, worth 2m/-.

The patrol team comprised of ward fisheries officers, village and ward executive officers, and district task force against illegal fishing.

"This is a non-stop operation till the illegal practices have stopped. We are very committed to this and nobody will be spared. We've informers everywhere, and they informed us also thus lead to the arrest of these suspects," said Nguvila.

Nguvila warned that, if there are tycoons who sponsor the illegal fishing, that their days were numbered.

He also warned the task force not to engage in any way in the illegal business saying once found; stern measures will be taken against them.

Muleba district fisheries officer, Wilfred Tibendelana said illegal fishing has massively contributed to the depletion of fish stocks, and the government has been mounting regular operations in the Indian Ocean, lakes and rivers.

Scanned with CamScanner